

TAARIFA YA ZIARA YA WAZIRI WA ARDHI NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI WILAYA YA NGARA MHE WILLIAM VANGIMEMBE LUKUVI TAREHE 22/02/2018

Waziri wa ardhi nyumba na maendeleo ya makazi Mheshimiwa William Vangimembe Lukovi (MB) Alitembelea Wilaya ya Ngara tarehe 22/02/2018. Lengo la ziara yake lilikuwa kusikiliza matatizo ya wananchi yanayohusu ardhi na kushirikiana nao kuyatafutia ufumbuzi. Katika ziara yake waziri alipokea taarifa ya Wilaya kuhusu maendeleo ya ardhi na kujadili. Aidha alihutubia mkutano wa hadhara kwenye Mji wa Benaco na kwenye hadhara hiyo alihojiana na mwananchi mmoja mmoja mwenye tatizo/mgogoro kuhusiana na ardhi kwa kurejea fomu walizojaza maarufu kwa jina la “Funguka kwa Waziri”.

YATOKANAYO NA TAARIFA YA WILAYA KUHUSU MAENDELEO YA ARDHI

1. Waziri aliona upungufu wa wataalam wa ardhi Wilaya ya Ngara na akamwagiza Kamishna msaidizi kanda ya ziwa amuhamishe Kaimu Afisa Ardhi Mteule ambaye yuko Mwanza kwenye ofisi ya kanda kuja Halmashauri ya Wilaya ya Ngara.
2. Waziri aliona kuwa Wilaya ya Ngara iko nyuma sana kwenye suala la upimaji na utoaji wa hati miliki hali ambayo inasababisha watu kutokulipa kodi ya pango la ardhi. Aidha alieleza kwamba Wizara yake imesajili zaidi ya kampuni sitini za upimaji hivyo Halmashauri itumie fursa hiyo kupanga miji yake na kuhakikisha watu wanapata hati miliki za ardhi yao. Aidha ameagiza Halmashauri iainishe maeneo yote yenyetabia ya kimiji haraka na kuomba yatangazwe kuwa maeneo ya mipango miji ili yapangwe mapema. Amesema pia kuwa Sekta ya ardhi itanunua vifaa vya kisasa vya upimaji ili kuharakisha upimaji wa ardhi nchini.
3. Waziri ameagiza kwamba kamishna Msaidizi kanda ya Ziwa aje Ngara kupekua mashamba yote makubwa (zaidi ya ekari 50) ambayo yana hati miliki na kama yana sifa ya kufutwa utaratibu ufuatwe yafutwe.
4. Kwa mashamba makubwa (zaidi ya ekari 50) 12 yaliyofutiwa umiliki na vijiji kwa kutofuata kanuni taratibu na sheria za ardhi ameagiza Mchakato wa maombi uanzu upya. Maombi yajadiliwe kwenye kikao cha Serikali ya Kijiji na Mkutano Mkuu wa kijiji na Mkuu wa Wilaya lazima ashirikishwe kwenye mikutano hiyo. Kama mkutano mkuu utaridhia, mchakato wa kupata hati uendelee ili wahusika walipe kodi ya ardhi. Shughuli hii iwe imekamilika mwishoni mwa mwezi Mei 2018.
5. Migogoro ya nchi na nchi: Waziri alieleza kwamba serikali ya awamu ya tano inatarajia kumaliza mgororo iliyopo kwa kutumia alama zinazoonekana “PILLARS” kwenye nchi kavu. Aidha serikali itatutumia mfumo wa “KIELEKTRONICS” kwenye mito na maeneo chepechepe/tingatinga.

6. Mgogoro wa mpaka kati ya Wilaya ya Ngara na Wilaya ya Biharamulo eneo la Nyabiondo na Keza.

Mhe waziri alielezwa kwamba wataalam wa ardhi ngazi ya Mkoa na Wilaya zote mbili walitembelea mpaka na kutafsiri gazeti la serikali la eneo husika (GN Na.185) kwa viongozi na wananchi wa Wilaya zote mbili ikaonekana mipaka iko sahihi. Ila wananchi wanaoishi kwenye kitongoji cha Nyabiondo na Mlore wanapenda watambulike kama wananchi wa Ngara kwa kuwa huduma zote wanapata Ngara. Mhe. Waziri alieleza kuwa suala la kubadilisha mpaka kati ya Wilaya na Wilaya mapendekezo yanatakiwa yatoke kwenye Wilaya husika

MKUTANO WA HADHARA

Katika mukutano wa hadhara uliofanyika kwenye mji mdogo wa Benaco Waziri wa Ardhi nyumba na maendeleo ya makazi aliwaeleza wananchi kuwa serikali imepanga kuhakikisha makazi ya wananchi yamerasimishwa na kupatiwa hati miliki ya miaka 99. Aliwaeleza pia wananchi kuwa sheria ya nchi hairuhusu wageni kupewa ardhi kama ilivyo kwa wazawa. Hivyo kama kuna mgeni ye yeyote aliyepewa ardhi anyang'anywe. Wageni wanaotaka kupata Ardhi Tanzania wapitie mlango wa uwekezaji ili wapewe hati ya uwekezaji. Aidha aliwaahidi wananchi kwamba atamleta Afisa Ardhi Mteule ili aharakishe shughuli ya kuwaandalia wananchi hati miliki za Ardhi.

MAHOJIANO MAELEKEZO NA USHAURI WA WAZIRI KWA KUTUMIA FOMU ZA “FUNGUKA KWA WAZIRI”

Waziri wa ardhi Nyumba na Maendeleo ya makazi alihojiana na wananchi takribani 148 akatoa maamuzi, maelekezo na ushauri mbalimbali kama inavyoonekana kwenye jedwali. Baada ya kumaliza mahojiano na wananchi waliojaza fomu za “Funguka kwa Waziri” alifunga kwa kusisitiza mambo yafuatayo:

1. Halmashauri ya Wilaya ipange ratiba ya kusikiliza mashauri kwenye kata mbalimbali.
2. Watu wote wenye mashamba yenyе ukubwa zaidi ya ekari 50 wafanye mchakato wa uhawilishaji wapatiwe hati miliki ili walipe kodi. Mchakato ukamilike kabla ya mwisho wa mwezi Mei 2018.
3. Kama wananchi watakataa kumpa muombaji idhini ya kupatiwa hati miliki lazima Wilaya/Serikali ishiriki kugawa na kupanga matumizi ya maeneo hayo.
4. Uthamini wa maeneo yanayopangwa kuwa miji ufanyike kabla ya kugawa viwanja ili kupunguza/ kuondoa migogoro isiyokuwa ya lazima. Halmashauri itumie stakabadhi mbili (1. Ya gharama za Halmashauri na 2. Gharama za upimaji